

## COUNTY GOVERNMENT OF LAMU



## THE COUNTY ASSEMBLY OF LAMU

### THE HANSARD

Thursday, 2<sup>nd</sup> October, 2025

*The Assembly met at the  
Main Chambers, at 2:30 p.m.*

[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna) in the Chair]

#### PRAYERS

**[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]:** Next Order.

**Clerk-at-the-Table:** Notices of Motion

#### NOTICES OF MOTION

**[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]:** Honorable Members, since Honorable Mercy and Honorable Beatrice are not in the House I defer these Notices of motion in the next Sitting.

**[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]:** Next Order.

**Clerk-at-the-Table:** Statements.

**STATEMENTS***food shortage in Schools*

**MCA Barisa Deko Bana (Basuba):** Thank you Mr Deputy Speaker. Mr Deputy Speaker Sir, Pursuant to Standing Order 41(2)(C) I wish to request for a Statement from the Chairperson of the Departmental Committee on Education, Culture and Social Welfare on matters pertaining food shortage in Schools majority inhabited by the minority communities in Lamu County.

Mr Deputy Speaker Sir, I rise to bring to the attention of this Honorable House a matter of grave concern affecting our Schools located in areas inhabited by the Boni and Awer minority communities within Lamu County.

Mr Deputy Speaker Sir, the Boni and Awer are recognized as marginalized communities that deserve special attention and protection under the Constitution of Kenya. In recognition of their disadvantaged status, its the responsibility of the County Government of Lamu to ensure that schools within these communities are fully sponsored, including the provision of adequate food supplies for learners.

Mr Deputy Speaker Sir, it is disheartening to note that most schools serving these communities i.e Mokowe Arid Zone, Pandanguo, Bahati Njema and Witu Boarding Schools are currently experiencing a severe shortage of food. This situation has exposed learners to hunger, absenteeism and in some cases dropout from school. It has also undermined the National and County Government's efforts toward improving education standards and securing the future of our children.

Mr Deputy Speaker Sir, the school feeding programs are not merely supplementary they are lifeline for children in marginalized communities where poverty levels are high and alternative source of nutrition are

limited. Denying these students to daily meals in Schools is equivalent to delaying them the right to education and survival.

Mr Deputy Speaker Sir, I therefore urge this House to take up this matter with urgency and call upon the County Executive Committee Member (CECM) in charge of Education as well as that of Finance to immediate address the shortage of food in these Schools and put in place sustainable measures to ensure uninterrupted food feeding program in Boni and Awer areas.

Mr Deputy Speaker Sir, it is our moral and constitutional duty to safeguard the welfare of these minority community and ensure that no child is left behind in access to education.

Mr Deputy Speaker Sir, I seek to know from the Chairperson of the Departmental Committee on Education, Culture and Social Welfare:-

1. What immediate intervention has the Department of Education put in place to ensure that learners in these Schools are not subjected to hunger and absenteeism?
2. When will the Committee summon the CECM for education and CECM for Finance to clear the issue pertaining the feeding program for the Boni and Awer area?
3. How does the County Government plan to collaborate with the National Government and development partners to supplement effort in ensuring children from Boni and Awer Communities access adequate nutrition in Schools?

**[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]:** I can see the Chair and Vice are not in the House. Do we have any Member? If we don't have, Chief Whip can you follow up that matter.

**MCA Suleiman Mohamed Farah (Witu):** Asante sana Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika kwa niaba ya Kamati ningeomba nipewe muda wa wiki moja.

**[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]:** Next Statement.

*Water shortage in Kizingitini.*

**MCA Barisa Deko Bana (Basuba):** Thank you Mr Deputy Speaker. Mr Deputy Speaker Sir, on behalf of Honorable Amina I rise Pursuant to Standing Order 41(2)(C) to seek a Statement from the Chairperson of the Departmental Committee on health services, water and environment on matters regarding the water shortage in Kizingitini.

Mr Deputy Speaker Sir, for prolong period the people of Kizingitini have been grappling with adequate water scarcity. This has severely

**[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]:** Response from the Chairperson of the Departmental Committee on health services, water and environment.

**MCA Francis Ngure Gakonga (Bahari):** Asante Bwana Naibu Spika, ningeomba nipewe muda wa wiki mbili ili nije na majibu sahihi.

**[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]:** Next Order.

**Clerk-at-the-Table:** Motion.

### **MOTION**

*Establishment of a new livestock (Animal) market in Lamu County*

**MCA James Njaaga Kariuki (Hindi):** Thank you Mr Deputy Speaker. Mr Deputy Speaker Sir, I beg to move the following motion:

**AWARE THAT**, agriculture and livestock development including animal markets are fully devolved functions under part 2 of the Fourth Schedule of the Constitution of Kenya (2010).

**FURTHER AWARE THAT**, a large population in Lamu County especially in Wards such as Witu, Mkunumbi, Hindi, Bahari, Basuba and Kiunga depend on livestock keeping as a primary source of income and livelihood.

**RECOGNIZING** the growing need for formal, regulated and accessible livestock trading spaces that will support the sale and movement of cattle, goats, sheep and camels.

**NOTING** that existing livestock markets in the County are few, often informal, poorly equipped and located far from major livestock-producing areas, forcing farmers to travel long distances and incur high transportation costs.

**CONCERNED** that the lack of adequate and accessible animal markets contributes to:

- Unfair pricing and exploitation of local livestock keepers.
- Spread of livestock diseases due to lack of veterinary inspection points.
- Missed economic opportunities for local traders, youth and women and
- Reduced revenue collection by the County Government.

**THIS HONORABLE ASSEMBLY RESOLVES THAT:**

- 1.** The County Executive Committee Member (CECM) in charge of Agriculture, Livestock and Fisheries in consultation with stakeholders, identifies and sets aside land for the establishment of

a new, modern animal market in a strategic location that serves multiple livestock-producing Wards.

2. The market should be equipped with appropriate facilities including:
  - Holding pens and shaded areas,
  - Loading and offloading ramps,
  - Watering points and sanitation facilities,
  - Veterinary inspection units and
  - Revenue collection booths.
3. The County Executive ensures that the market is:
  - Zoned and gazetted as a legal trading point.
  - Designed in consultation with local livestock producers, traders and veterinary professionals and
  - Developed with a clear maintenance and management plan, possibly through cooperatives or public-private partnerships (ppp).
4. The Department of Finance and Economic Planning allocates funds in the next financial year for the planning, design and phased construction of the new animal market.
5. The CECM provides a progress report to this Assembly within 60 days of the adoption of this motion, outlining steps taken toward implementation.

I therefore Mr Deputy Speaker Sir, call this Honorable House to adopt this motion which will actually be of benefit to our County. It is my pleasure to call Honorable Gakonga to second.

*Secunder*

**MCA Francis Ngure Gakonga (Bahari):** Asante sana Bwana Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii. Bwana Naibu Spika nimesimama kuunga mkono mada iliyoletwa na Mheshimiwa James njaaga na nakumbuka wakati wa Serikali ya Ugatuzi ilipoanzishwa 2013 mojawapo wa mambo ambayo yanashughulikiwa kwa kuleta ugatuzi ni kuhakikisha ya kwamba huduma

*Disclaimer: The electronic version of the Assembly Hansard Report is for information purpose only. A certified version of this Report can be obtained from the Office of the Clerk.*

zinapatikana karibu na wananchi. Kwa hivyo uwepo wa soko moja katika Kaunti yetu ya Lamu ni sawa na kuwanyima wananchi haki zao za kiuchumi.

Bwana Naibu Spika soko ambalo linazungumzia hapa litakuwa soko la kisasa ambalo litakuwa na vibanda vya kuhifadhi wanyama tofauti tofauti. Pia litahitaji mahali pa malisho na kivuli cha kuwakinga wanyama wasipate jua na mvua. Soko hilo hilo litahitaji huduma za madaktari wa wanyama ili waweze kuwatibu wanyama hao.

Bwana Naibu Spika pia kunafaa kuwe na sehemu maalum pakuwapakia wanyama hao baada ya kununuliwa ili kuweza kuwasafirisha kwa uzuri. Soko hilo linafaa kuwa na mpangilio mzuri wa usafi pindi wanyama hao watakapotupa vinyesi vyao. Kwa hivyo ningeiomba idara husika izunguke Wadi zote na ifanye utafiti wa kujua ni Wadi ngapi zinafuga wanyama ili kuwasaidia wakulima ambao wanafanya ufugaji.

#### Motion Proposed

#### Members Contributions

**MCA Suleiman Mohamed Farah (Witu):** Asante sana Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika nimesimama kwa kupinga mswada ulioletwa na Mheshimiwa James Njaaga. Nashangaa katika Wadi yangu kuna soko lakini haitumiki bali tunawasafirisha wanyama na kuwapeleka katika soko la Garsen. Kwa hivyo ningelipenda Bunge hili badala ya kujenga soko jipya katika Wadi yangu tuweze kulitilia maanani soko lile la zamani.

**MCA John Mburu Gitonga (Hongwe):** Asante sana Bwana Naibu Spika kwa kunipa nafasi ya kuunga mkono kwa sababu soko hili litaweza kuwasaidia wakaazi wa Lamu tukizingatia ya kwamba wengi ni wafugaji. Kwa hivyo ujenzi wa soko lengine katika Kaunti yetu ya Lamu utaweza kuboresha uchumi.

**MCA Shekhuna Abbas Shekhuna (Mkomani):** Asante sana Bwana Naibu Spika kwa kunipa nafasi ya kuunga mswada ulioletwa na Mheshimiwa James Njaaga. Mswada huu unahuzunisha kwa sababu wanyama hawawezi kuzungumza na kama wangepewa muda wa kuzungumza basi hawangetamani kuletwa ulimwenguni. Kwa hivyo wanafaa kuchungwa vizuri kwa kujengewa soko la kuwahifadhi wanyama hao kwa sababu hata wao wanalipiwa ushuru na wahusika.

MCA Barisa Deko Bana (Basuba): Asante sana Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika nimesimama kuunga mkono mswada ulioletwa na James Njaaga na ninaona amekuja na fikra nzuri sana. Na ninaona Wizara ya mifugo haikuweza kuleta fikra mbadala ya kuwahifadhi mifugo iliyoko katika Kaunti yetu ya Lamu. Vilevile kutakuwa na nidhamu wa ununuzi wa mifugo hiyo ambapo mnunuzi atakwenda kununua sokoni badala ya uwanjani.

#### Mover's Response

**MCA James Njaaga Kariuki (Hindi):** Asante sana Bwana Naibu Spika, pili ningependa kutoa pongezi kwa Waheshimiwa waliochangia mswada niliokuja nao. Na pia kuzingatia maoni ya aliyeupinga mswada huu. Kusema kweli Kaunti yetu ya Lamu inaendelea kukua na ndiposa nikaona kuna umuhimu wa kuja na wazo hili. Na kuna wakulima wana mifugo na wangependa kuiuza lakini wanakosa soko la kwenda kuwauza mifugo yao na ukizingatia ya kwamba wanajipatia riziki zao kupitia mufugo hiyo.

Kwa hivyo ni wakati mwafaka wa kuwatetea wafugaji hawa ili wapate haki zao za kiuchumi na Serikali yetu ya Lamu itaweza kupata ushuru kupitia wanyama hao na kuimarisha uchumi wetu.

(Question put and agreed upon)

**[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]:** Next motion

---

**No. 104**

---

*APPROVAL OF THE REPORT OF THE DEPARTMENTAL COMMITTEE ON LANDS, PHYSICAL PLANNING AND HOUSING ON THE VETTING OF THE MUNICIPALITY BOARD MEMBER NOMINEE, MR MOHAMED YUSUF NOOR*

**MCA Suleiman Mohamed Farah (Witu):** Thank you Mr Deputy Speaker. Mr Deputy Speaker Sir, I beg to move the following motion:

**THAT,** Pursuant to the provision of Constitution of Kenya, County Government Act No 17 of 2012 and the County Assembly Standing Order this House adopt the report of the Departmental Committee on Lands, Physical Planning and Housing on the vetting of Lamu Municipality Board Member Nominee, Mr Mohamed Yusuf Noor laid on the Table of the House on Tuesday 30<sup>th</sup> September 2025.

*Secunder*

**MCA Barisa Deko Bana (Basuba):** Asante Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika nachukua fursa hii kuweza kueleza manufaa ya Bwana Mohamed Yusuf Noor. Kama tujuavyo kulikuwa na pengo katika Bodi ya Manispaa lakini kwa saa hii naona Bodi imekamilika. Kwa hivyo ningependa kuipongeza kamati ya ardhi kwa kutupa kipaumbele sisi watu wa Basuba. Bwana Naibu Spika, Mohamed Yusuf Noor ni kijana mwenye bidii na ana uwezo wa kufanya kazi na vilevile ni Meneja wa kamati ya Awer katika Wadi yangu ya Basuba. Kwa hivyo itakuwa ni wakati mwafaka kwa sisi watu wa Basuba kuwa katika Bodi ya Manispaa ya Lamu. Nikiwa Mwakilishi wa Wadi ya Basuba nimefurahi sana na nina Imani watu wangu watafaidika iwapo huu mswada utapita. Na vilevile ningependa kuwahimiza Wajumbe wenzangu waweze kuunga mkono mswada huu ili kamati husika ifanye kazi yao na tuweze kusonga mbele kimaendeleo.

Motion Proposed

**Members Contributions**

---

*Disclaimer: The electronic version of the Assembly Hansard Report is for information purpose only. A certified version of this Report can be obtained from the Office of the Clerk.*

**MCA James Njaaga Kariuki (Hindi):** Asante sana Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika ningependa kuipongeza kamati ya mashamba kwa kuweza kumpitisha Mohamed Yusuf Noor na ninaona wamefanya jambo la busara na ni lazima kazi ifanyike ili Kaunti yetu ya Lamu iweze kusonga mbele kimaendeleo.

**MCA Shekhuna Abbas Shekhuna (Mkomani):** Asante sana Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika, ninaona kamati ya ardhi imefanya jambo la busara kwa kumchagua Mohamed Yusuf Noor kama Mwanakamati wa Manispaa ya Lamu baada ya kumfanyia ukaguzi wa kutosha na kumuona anafaa. Na nina Imani atafanya kazi zake vizuri.

#### Mover's Response

**MCA Suleiman Mohamed Farah (Witu):** Asante Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika ningependa kuishukuru Ofisi yako na Ofisi ya Karani Mkuu kwa kutupa nafasi sisi Wanakamati wa kamati ya ardhi kwenda kuikalia hii ripoti. Na sisi kama wanakamati tukaamuwa kuipa kipaumbele jamii ambayo ina wapiga kura wachache sana na nina Imani itakuwa furaha kubwa kwa jamii ya Awer kwa kupata Mwakilishi wa Bodi ya Manispaa ya Lamu na ninajuwa hawatadhulumika tena kimaendeleo. Na vilevile Mheshimiwa Barisa Deko ataweza kujifakhari kwa watu wake kuwa wamepata mtetezi.

(Question put and agreed upon)

#### **ADJOURNMENT**

**[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]:** Honorable Members, there being no other business, the Assembly stands adjourned until Tuesday 7<sup>th</sup> October 2025 at 2:30pm.

*The Assembly rose at 4:30pm*